

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**YATOKANAYO NA KIKAO KWANZA**

**06 NOVEMBA, 2018**

## **MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 06 NOVEMBA, 2018**

### **I. WIMBO WA TAIFA NA DUA**

Saa 3.00 Wimbo wa Taifa uliimbwa na kisha Mhe. Job Y. Ndugai (SPIKA) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

MAKATIBU MEZANI:

- i. Ndg. Stephen Kagaigai
- ii. Ndg. Ramadhan Issa
- iii. Ndg. Joshua Chamwela
- iv. Ndg. Ruth Makungu

### **II. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Wabunge wafuatao waliapa Kiapo cha Uaminifu:-

1. Mhe. Julius Kalanga Laizer;
2. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara;
3. Mhe. Timotheo Paul Mnzava; na
4. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka.

### **III. TAARIFA YA SPIKA:**

Mhe. Spika alitoa Taarifa kuhusu Sheria zilizo pata kibali cha Rais kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi Na. 5 ya Mwaka 2018 [*The Dodoma Capital City (Declaration) Act, No. 5 of 2018*];

- (ii) Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania Na. 6 ya Mwaka 2018 [*The Tanzania Teacher's Professional Board Act, No. 6 of 2018*];
- (iii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) Na. 7 ya Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, No. 7 of 2018*];
- (iv) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) Na. 8 ya Mwaka 2018 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, No. 8 of 2018*];
- (v) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Na. 9 ya Mwaka 2018 [*The Public Private Partnership (Amendment) Act, No. 9 of 2018*].

#### **IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

- (i) Naibu Waziri wa Fedha Na Mipango aliwasilisha Mezani Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- (ii) Mhe. Maria Ndila Kangoye aliwasilisha Mezani Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020;
- (iii) Mhe. Masoud Abdallah Salim aliwasilisha Mezani Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020.

**V. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Swali Na. 1: Mhe. Esther Michael Mmasi

Nyongeza: Mhe. Esther Michael Mmasi  
Mhe. Mussa Azzan Zungu

Swali Na. 2: Mhe. Abdallah Ally Mtolea

Nyongeza: Mhe. Abdallah Ally Mtolea

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na. 3: Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza

Nyongeza: Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza  
Mhe. Catherine Valentino Magige

Swali Na. 4: Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

Nyongeza: Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Swali Na. 5: Mhe. Edward Franz Mwalongo

Nyongeza: Mhe. Edward Franz Mwalongo

**WIZARA YA KILIMO:**

Swali Na. 6: Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab

Nyongeza: Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab

Swali Na. 7: Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

Nyongeza: Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Swali Na. 8: Mhe. Tunza Issa Malapo

Nyongeza: Mhe. Tunza Issa Malapo

Swali Na. 9: Mhe. Josephine Johnson Genzabuke

Nyongeza: Mhe. Josephine Johnson Genzabuke

**WIZARA YA NISHATI:**

Swali Na. 10: Mhe. Augustino Vuma Holle

Nyongeza: Mhe. Augustino Vuma Holle  
Mhe. Hussein Mohammed Bashe  
Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako

Swali Na. 11: Mhe. Musa Rashid Ntimizi

Nyongeza: Mhe. Musa Rashid Ntimizi  
Mhe. Mwita Mwikabe Waitara

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na. 12: Mhe. Peter Ambrose Lijualikali

Nyongeza: Mhe. Peter Ambrose Lijualikali

Swali Na. 13: Mhe. Hassan Seleman Kaunje

Nyongeza: Mhe. Hassan Seleman Kaunje

## **MATANGAZO**

1. Mhe. Spika aliwakumbusha Wabunge kurejea na kuzingatia Kanuni za Bunge;
2. Swali lolote la nyongeza lazima liendane na swali la msingi;
3. Kama kuna tuhuma nzito kama alizotoa (Mhe. Genzabuke) njia inayopaswa kufuata ni kutoa taarifa kwa Waziri Mkuu au Spika ili hatua stahiki zichukuliwe na si kusubiti muda wa maswali ndiyo aulize swali;
4. Wabunge wote wanatambuliwa kwa Majimbo, Kuteuliwa na Viti Maalum;
5. Wabunge waliokuwa wagonjwa kwa muda mrefu i.e. Mhe. Timbe alipewa pole na kukaribishwa Bungeni.

## **WAGENI:**

1. Wageni wa Mhe. Julius Kalanga Laizer walitambuliwshwa wakiongozwa na Mke wake Mama Sara.
2. Wageni wa Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara ambao ni Viongozi na Wanachama wa CCM kutoka Dar es Salaam.
3. Wageni wa Mhe. Timotheo Paul Mnzava wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mhe. A. Mnyeti.
4. Wageni wa Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka kutoka Liwale walitambulishwa.
5. Wageni wa Mhe. Naibu Spika kutoka Mbeya walitangazwa.
6. Wageni wengine wote waliokuwa Ukumbini walitambulishwa.

## MATANGAZO MENGINE

1. DODOMA MARATHON inaomba Wabunge watakaoshiriki mbio za Hisani tarehe 10 Novemba, 2018 waorodheshe majina yao mapokezi.
2. Wabunge walitangaziwa kushiriki Chanjo ya Homa ya Ini katika Mkutano huu wa 13 unaoendelea.
3. Wabunge walitangaziwa kuhudhuria Ibada *chapel* ya Bunge saa 7.00 mchana baada ya Bunge kusitishwa.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa Mwaka 2018 (*The Microfinance Bill, 2018*).

**(Kusomwa Mara ya Kwanza)**

## MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. Joseph Kasheku Msukuma alitumia Kanuni ya 68 (7) aliomba mwongozo kuhusu upande wa upinzani kutamka “atambulishwe Mke wa Dodoma” wakati Spika akimtambulisha Mke wa Mhe. Mwita Mwikabe Waitara kwamba kitendo hicho si kizuri kinavuruga faragha na kinaweza sababisha migogoro katika familia.
2. Mhe. Pascal Haonga aliomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68 (7) kuhusu swali la nyongeza namba 9 kutojibiwa vizuri. Hata hivyo Spika aliukataa mwongozo wake kwa kuwa hata swali la nyongeza la Mhe. Josephine Johnson Genzabuke lilikataliwa na Kiti.

## VI. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango alitoa Hoja kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo

wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

Hoja iliungwa mkono na kuafikiwa.

## **VII. KAMATI YA MIPANGO:**

Bunge liliingia kwenye Kamati ya Mipango.

- (i) Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. George Boniface Simbachawene aliwasilisha Taarifa ya kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2010.
- (ii) Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha Mhe. Halima James Mdee aliwasilisha Bungeni Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2010.

## **VIII. BUNGE KUREJEA**

### **IX. KUSITISHA BUNGE:**

Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni.

### **X. BUNGE KUREJEA:**

Saa 11.00 Bunge lilirejea likiongozwa na Mhe. Mussa A. Zungu (Mwenyekiti wa Bunge).



## HOJA ZA SERIKALI – KAMATI YA MIPANGO

Mjadala kuhusu Hoja ya Waziri wa Fedha na Mpango juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo uliendelea na Bunge lilikaa kama Kamati ya Mpango na wafuatao kuchangia:-

|   |   |                       |
|---|---|-----------------------|
| 1. Mhe. Hassan Elias Massala                      | - | CCM                   |
| 2. Mhe. George Malima Lubeleje                    | - | ccm                   |
| 3. Mhe. Allan Joseph Kiula                        | - | CCM                   |
| 4. Mhe. Riziki Said Lulida                        | - | CUF                   |
| 5. Mhe. Jitu Vrajlal Soni                         | - | CCM                   |
| 6. Mhe. Steven Lemomo Kiruswa                     | - | CCM                   |
| 7. Mhe. Mch. Peter Somon Msigwa                   | - | CHADEMA               |
| 8. Mhe. Musa Rashid Mtimizi                       | - | CCM                   |
| 9. Mhe. Selemani Jumanne Zedi                     | - | CCM                   |
| 10. Mhe. Anthony Ekalist Komu                     | - | CHADEMA               |
| 11. Mhe. Zainab Matitu Vullu                      | - | CCM                   |
| 12. Mhe. Salum Meinyi Rehani                      | - | CCM                   |
| 13. Mhe. Lucia Michael Mlowe                      | - | CHADEMA               |
| 14. Mhe. Augustino Manyanda Maselle               | - | CCM                   |
| 15. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau                      | - | CCM                   |
| 16. Mhe. Frank George Mwakajoka                   | - | CHADEMA               |
| 17. Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele<br>na Uchukuzi | - | Waziri wa Mawasiliano |
| 18. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula               | - | CCM                   |

Kamati ya Mipango kusitishwa na Bunge kurejea.

### **XI. KUAHIRISHA BUNGE:**

Saa 2.00 Usiku Mwenyekiti wa Bunge aliahirisha Bunge hadi siku ya Jumatano tarehe 07/11/2018 saa 3.00 Asubuhi.